

TANGAZO KUHUSU MALIPO YA POSHO ZA 'INTERNS' 2015/2016

Napenda kuwataarifu kuwa, barua zilizotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii za kupangiwa vituo vya kufanyia Mafunzo kwa vitendo kwa 'Interns', zilikuwa na dosari katika **Viwango vya Posho** zinazostahili kulipwa kwa kila mwezi kwa kipindi chote cha mafunzo hayo.

Utaratibu unaotumika kwa sasa ni kumlipa 'Intern' asilimia **themanini (80%)** ya mshahara wa mwezi wa Mwajiriwa wa Kada husika. Hivyo, kwa madhumuni ya kurekebisha dosari hizo **Waganga Wakuu/Wafawidhi wote wa Hospitali** ambazo zimepokea 'Interns' wanaarifiwa kuzingatia viwango vifuatavyo kulingana na Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 1 wa Mwaka 2015 kuhusu Marekebisho ya Mshahara kwa Watumishi wa Umma kama ilivyoainishwa hapa chini:-

Na.	Kada	Ngazi ya Mshahara	Mshahara	80% ya Mshahara
1.	Daktari	TGHS E	1,480,000/=	1,184,000/=
2.	Mfamasia	TGHS D	1,215,000/=	972,000/=
3.	Afisa Mteknolojia	TGHS C	980,000/=	784,000/=
4.	Afisa Muuguzi	TGHS C	980,000/=	784,000/=

Ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wa malipo husika **Waganga Wakuu/Wafadhili mnatakiwa kuwataarifu 'Interns' wote** dhidi ya marekebisho haya mapema.

**KATIBU MKUU,
WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII,
S.L.P. 9083,
6 BARABARA YA SAMORA MASHEL,
11478 DAR ES SALAAM.**